



TAARIFA YA TAHADHARI KWA WANACHAMA KUSUDIO LA SCANCEM INTERNATIONAL DA YA KUNUNUA ASILIMIA 68.33 ZA TANGA KUTOKA AFRISAM MAURITIUS INVESTMENT HOLDINGS LIMITED

TANGA CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY (DSE: TCPLC) (Imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) ("Tanga" au "Kampuni")

Wanahisa wanakumbushwa kuhusu tangazo lililotolewa na HeidelbergCement AG ("Heidelberg Cement") na AfriSam Mauritius Investment Holdings Limited ("AfriSam") tarehe 26 Oktoba 2021 (tangazo la HeidelbergCement) ambapo ilitangazwa kuwa Scancem International DA ("Scancem"), kampuni tanzu ya HeidelbergCement, na AfriSam wamekamilisha makubaliano ambapo Scancem itanunua asilimia 68.33 ambazo ni hisa za AfriSam ndani ya Tanga Cement PLC, ("Mnunuzi"). Wanahisa wanahimizwa kusoma matangazo ya pamoja yanayotolewa na AfriSam na HeidelbergCement.

Bodi ya wakurugenzi ya Tanga ("Bodi") ilifahamishwa vyema na AfriSam kuhusu mapatano ya uuzwaji muda mfupi baada ya makubaliano kukamilika. Kwasasa Bodi itachukua na kufuata ushauri muafaka na kufuata hatua zinazohitajika kwenye masuala ya Soko la Mitaji na Dhamana na kufuata kanuni za (Ununuzi wa kuchukua, Uchukuaji na Muunganisho) za mwaka 2006. Bodi itatoa maelezo zaidi kwa wanahisa wake kwa wakati muafaka kuhusu suala hili.

Ununuzi utategemea kutimizwa, au ikiwezekana, kuondolewa kwa masharti ("Masharti") ifikapo tarehe 30 Juni 2022 au tarehe ya baadaye endapo wahusika watakubaliana kimaandishi. Masharti haya yamewekwa kwa kina katika tangazo la pamoja baina ya AfriSam na HeidelbergCement. Bei elekezi kwa kila hisa itakayolipwa na Scancem kwenda AfriSam ni Tzs 3,157 kwa hisa ya Tanga ("Bei ya Ununuzi"). Bei ya Ununuzi pia inategemea marekebisho yanayoendana na deni, mtaji wa kufanyia kazi na gharama nyingine. HeidelbergCement na AfriSam inatahadharisha kuwa hakuna uhakika wa makubaliano ya Bei ya mwisho ya Ununuzi.

Endapo ununuzi huu utakuwa bila ya masharti na kutekelezwa, Scancem itachukua udhibiti wa kampuni. Endapo hili litatokea, Scancem itatoa ofa ya jumla ya ununuzi wa hisa zilizobakia za Tanga ("Ofa ya Jumla"); hilo litafanyika baada ya kufikiwa kwa makubaliano ya mwisho ya ununuzi, na bei itafahamika.

Wanahisa wanatahadharishwa kuwa hakuna uhakika kwamba masharti yote ya ununuzi yatatekelezwa au kushindikana. Hivyo, hakuna uhakika kuwa ofa ya jumla itatolewa. Vilevile hakuna uhakika wa makubaliano ya bei ya mwisho ya ununuzi.

Kampuni bado inaendelea kufanya biashara huku kukiwa na tangazo la tahadhari lilitolewa mnamo tarehe 31 Agosti 2021. Wanahisa wanashauriwa kuendelea kuwa wangaalifu wanapojishughulisha na biashara ya dhamana za Tanga.

Taarifa zaidi zitaendelea kutolewa kwa muda muafaka.

Kwa niaba ya Bodi

Mwenyekiti wa Bodi
Chairman of the Board
27 Oktoba 2021